*Kioo cha Lugha, Juz. 21(1), 92-106*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v21i1.6

# Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili

*Stella Faustine*[1]

## Ikisiri

Mijadala mbalimbali imefanywa na wataalamu na wahakiki wa kazi za fasihi kuhusu mtindo wa uhalisiajabu. Miongoni mwake ni ile inayobainisha chanzo chake katika fasihi ya Kiswahili, athari za matumizi yake, na namna inavyoweza kuakisi hali halisi ya maisha katika jamii husika. Pamoja na mijadala hiyo kuweka misingi katika uelewekaji wa kazi za fasihi zinazotumia mtindo wa uhalisiajabu, suala la aina za mtindo wa uhalisiajabu halijajadiliwa kwa kuzingatia upekee na umuhimu wake. Makala hii imebainisha aina hizo kama zinavyojitokeza katika riwaya za Kiswahili za kihalisiajabu kwa kurejelea mifano kutoka riwaya za *Nagona* (Kezilahabi, 1990), *Bina – Adamu!* (Wamitila, 2002) na *Babu Alipofufuka* (Mohammed, 2001). Data ilikusanywa maktabani katika vitabu teule kwa kutumia mbinu ya usomaji wa matini. Uchambuzi, uhakiki na uwasilishaji wa data uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia kwa kutumia mkabala wa kitaamuli. Kwa kuzingatia kigezo cha kimaana, makala imebainisha aina sita za uhalisiajabu ambazo ni uhalisiajabu fantasia, tarazi, fifi, wa kimajazi, tashihisi na uhalisiajabu nasibishi.

## 1.0 Utangulizi

Uhalisiajabu ni dhana inayotokana na muunganiko wa maneno mawili, uhalisi na ajabu. Kwa mujibu wa BAKITA (2017), neno uhalisi hutumika kumaanisha hali ya kuwa bayana, yaani inayodhihirika katika maisha, na neno ajabu humaanisha jambo lisilomithilika au kuaminika. Katika makala hii, dhana ya uhalisiajabu imetumika kama mtindo katika fasihi ambapo mambo ya ajabu kama vile uchawi, fantasia na usawiri wa wahusika, mandhari na msuko wa matukio unaokiuka uhalisi huwekwa pamoja na yale ya kawaida katika kazi za fasihi ili kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira. Katika fasihi ya Kiswahili, mtindo huu ulianza kutumika katika fasihi simulizi na baadaye kushika kasi zaidi katika fasihi andishi kuanzia miaka ya 1960 mpaka hivi sasa. Kazi za *Nagona*, *Bina – Adamu!* na *Babu Alipofufuka* zinazohakikiwa katika makala hii ni miongoni mwa riwaya zilizoandikwa kwa kutumia mtindo huo.

Mtindo wa uhalisiajabu umezua mijadala mbalimbali miongoni mwa wataalamu wa fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya mijadala hiyo ni ile iliyofanywa na Mbatiah (1998) ambaye anazitazama kazi za *Nagona* na *Mzingile* kama kazi za

[1] Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania. Baruapepe: stelafau@gmail.com

kimajaribio kutokana na mtindo uliotumika. Kwa mtazamo wake, kazi hizo zinaonesha kuporomoka kwa ubunifu wa mtunzi kwani hazieleweki kwa hadhira kwa kiwango kikubwa. Senkoro (2007) amezitazama kazi zinazotumia mtindo wa kihalisiajabu kama kazi za kimajaribio ambazo zinajaribu kuchota vipengele vya fasihi simulizi na kuviingiza katika fasihi andishi. Anafafanua zaidi kuwa, uhalisiajabu ni mtindo mkongwe katika istilahi mpya kwani umekuwa ukitumika hapo awali katika fasihi simulizi. Madumulla (2009) anabainisha kuwa hakuna sababu ya kuziita kazi za uhalisiajabu kuwa ni za kimajaribio. Anatoa mifano yake kutoka katika riwaya za *Nagona* na *Mzingile* na kubainisha wazi kuwa, kazi hizo hazitoki nje ya mtazamo wa kidhanaishi wa mwandishi bali ni mwendelezo wa kazi zake za nyuma ambazo pia ziliandikwa kwa kukitwa katika mwegamo huo. Watafiti wengine waliotafiti kuhusu mtindo huo ni Faustine (2012 na 2021) ambaye ameangalia matumizi ya uhalisiajabu katika riwaya za Kezilahabi, na Angelus (2019) aliyetafiti kuhusu usawiri wa wahusika wa kihalisiajabu kwa kutoa mifano kutoka riwaya za Kezilahabi za *Nagona* na *Mzingile*.

Aidha, mijadala ya wataalamu hawa haijabainisha aina mbalimbali za mitindo ya uhalisiajabu katika fasihi ya Kiswahili. Jambo hili linatoa mwanya wa kufanyika kwa utafiti uliozalisha makala hii, ambao unabainisha aina mbalimbali za mtindo wa uhalisiajabu katika fasihi ya Kiswahili. Hii itasaidia kupanua mawanda ya kuelewa utajiri wa kazi za fasihi kifani na kimaudhui. Uandishi wa makala hii umegawanywa katika sehemu kuu sita. Sehemu ya kwanza ni utangulizi ambao unaeleza usuli wa mada. Sehemu ya pili inatoa muhtasari wa riwaya teule. Sehemu ya tatu inahusu methodolojia ya utafiti ambayo inatoa picha ya jumla ya namna mchakato mzima wa utafiti ulivyofanyika. Sehemu ya nne inahusu nadharia iliyotumika katika ukusanyaji na uchambuzi wa data. Sehemu ya tano ni mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Mwisho ni hitimisho la makala.

## 2.0 Muhasari wa Riwaya Teule

Sehemu hii inatoa muhtasari wa riwaya teule zilizotumiwa katika makala hii. Nazo ni *Nagona*, *Bina – Adamu!* na *Babu Alipofufuka*.

### 2.1 *Nagona*

*Nagona* ni riwaya iliyotungwa na E. Kezilahabi na kuchapishwa mwaka 1990. Hii ni riwaya iliyoandikwa kifalsafa kwa kutumia mtindo wa uhalisiajabu huku ikichimba na kuchambua masuala mbalimbali yahusuyo maisha. Mwandishi anaibua kitendawili kinachomtaka msomaji kutafakari maisha ni nini, yana thamani gani na mwisho wake ni nini. Aidha, anajenga tafakuri hiyo kwa kutumia dhihaka, kejeli, taswira, ishara na mafumbo ambayo ndani yake ndimo jibu la fumbo kuu kuhusu maisha linamopatikana.

Katika riwaya hii, anatumia sitiari kuu ya safari ambapo tunamwona mhusika Mimi akiwa safarini kuusaka ukweli wa maisha. Njiani, anakutana na mambo mengi ya kutisha na kuogofya kama vile kusikia sauti ya mtu akikohoa pasipo kuonekana (uk. 3), maiti kubeba Kurani na Biblia (uk. 4) na Mimi kupigwa na yaiviza pasipo kumwona mtu aliyempiga (uk. 5). Yote haya ni taswira anazotumia mtunzi ili kufikisha ujumbe wake kwa hadhira kuwa maisha ni safari ndefu yenye vikwazo vingi. Kitu cha msingi ni kuvishinda vikwazo hivyo na kuendelea na safari. Pia, kwa kutumia taswira ya Paa (uk. 67), anabainisha kuwa ukweli ni dhana telezi ambayo haikamatiki. Ukweli wa kipindi kimoja unaweza usiwe ukweli katika kipindi kingine. Vivyohivyo, ukweli kwa mtu mmoja unaweza usiwe ukweli kwa mtu mwingine. Yote haya anayawasilisha kupitia mtindo wa uhalisiajabu ambao unatumia taswira na ishara nyingi ili kuwasilisha ujumbe alioukusudia mwandishi.

## 2.2 *Babu Alipofufuka*

Riwaya ya *Babu Alipofufuka* imetungwa na S. A. Mohamed na kuchapishwa mwaka 2001. Hii ni miongoni mwa riwaya zinazowekwa katika mkondo wa fasihi za kimajaribio. Mwandishi anatumia mtindo wa uhalisiajabu kujadili matatizo mbalimbali yanayoukabili ulimwengu. Hoja muhimu anayojaribu kuiibua ni suala la kuwapo kwa mwanadamu, kutokuwapo kwake pamoja na uhusiano wake na watu na vitu vingine katika ulimwengu anamoishi (Faustine, 2017). Anatumia dhana za kufa na kufufuka kujadili mtazamo wa Waafrika kuhusu maisha yaliyokitwa katika duru ya kiwakati. Kwa kutumia mtindo wa uhalisiajabu, anaiwasilisha falsafa pana ya Waafrika kuhusu suala la maisha kuwa tupo, hatufi bali tunapita katika ulimwengu tuliomo kuelekea katika ulimwengu usioonekana wanakoishi wafu-hai.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, mwandishi anajadili mapokeo mbalimbali kiulimwengu kuhusiana na dhana ya utandawazi. Anaonesha namna utandawazi unavyoziathiri jamii mbalimbali ulimwenguni hasa nchi zinazoendelea. Wanajamii walio wengi wamesahau asili yao na kuanza kuiga kila wanachokiona pasipokujali misingi yao ya kimaadili. Kwa mfano, watu wa jinsi moja kuwa na uhusiano wa kimapenzi, ulawiti pamoja na binadamu kujamiiana na wanyama. Pia, ukiukwaji wa maadili katika suala zima la mavazi ni miongoni mwa mambo yanayojadiliwa na mwandishi (uk. 14). Kwa upande mwingine, anaonesha namna utandawazi ulivyosababisha watu kutoithamini asili yao na kudhani kuwa kila kilicholetwa na wageni ndicho kilicho bora zaidi. Hii inadhihirishwa na mhusika Bambo anayeona kuwa kujua lugha ya Kiingereza ndicho kigezo kinachodhihirisha ustaarabu na usomi wa mtu zaidi ya yule anayeongea lugha ya Kiswahili (uk. 41). Pia, mwandishi anakemea mambo yanayofanywa na viongozi wa Kiafrika kwa maslahi yao pasipo kujali maslahi ya umma. Amewataka kutekeleza misingi ya maadili ya uongozi kwa kuwathamini wale waliowapa dhamana ya kuongoza.

## 2.3 *Bina – Adamu!*

*Bina – Adamu!* ni riwaya iliyotungwa na K. W. Wamitila na kuchapishwa mwaka 2002. Hii ni miongoni mwa riwaya zinazowekwa katika tapo la fasihi ya kisasa kutokana na namna mwandishi anavyoifinyanga kazi yake kwa kutumia vionjo ya fasihi ya kisasa vinavyokiuka misingi ya uhalisi kama vile fantasia, mazingaombwe pamoja na ukatizwaji wa matukio. Mwandishi anatumia taswira na ishara mbalimbali zilizofumbatwa katika sitiari kuu ya kijiji pamoja a na safari ya Bina-Adamu Msafiri kueleza madhila mbalimbali yanayozikumba nchi zinazoendelea kisiasa, kiutamaduni na kiuchumi.

Kwa upande wa siasa, ameongelea masuala ya utawala na uongozi usiozingatia haki na usawa kwa raia uliokithiri. Badala ya viongozi hao kuwatumikia wananchi waliowapa dhamana ya kuongoza kwa uaminifu, wanatumia nafasi zao kujineemesha wao wenyewe (uk. 29).

Kwa upande wa uchumi, anaonesha ni namna gani mikataba mibovu na masharti magumu ya mikopo ya wawekezaji yanavyozididimiza nchi zinazoendelea na kuyaneemesha mataifa yaliyoendelea. Soko huria limekuwa kigezo cha kuchota bidhaa zenye thamani na kuyanufaisha mataifa yaliyoendelea huku nchi zinazoendelea zikibaki kuwa uwanja wa kuuzia bidhaa zisizo na ubora (uk. 51).

Kuhusu utamaduni, mwandishi ameonesha athari za utandawazi katika kudidimiza maadili ya jamii za Kiafrika. Katika ukurasa wa 88, anabainisha namna watu wanavyobaguana na hata kuuana kutokana na kuisahau misingi ya kimaadili ya dini zao. Yote haya, yanaelezwa kwa kutumia mtindo wa uhalisiajabu ambao unayakutanisha mambo yenye uhalisia na yale yanayokiuka misingi ya uhalisia na kuelezwa kama ni ya kawaida.

## 3.0 Methodolojia ya Utafiti

Utafiti huu ni wa maktabani na umekitwa katika usanifu wa kifani. Aina hii ya usanifu inahitaji kuwapo kwa namna fulani ya kuendana kwa jambo linalotafitiwa katika jamii au sehemu pana. Pia, huruhusu usampulishaji lengwa ili kupata watoataarifa/vitoataarifa kwa kuzingatia fani husika (Ponera, 2019). Usanifu huu ulimwezesha mtafiti kuteua vitoataarifa vya utafiti uliozalisha makala hii ambavyo vinaendana moja kwa moja na mada husika kimaudhui. Vitoataarifa katika makala hii ni riwaya tatu za kihalisiajabu ambazo ni *Nagona, Bina – Adamu!* na *Babu Alipofufuka*. Riwaya hizi ziliteuliwa mahususi kwa sababu ni riwaya zenye upevu mkubwa kisanaa; pia, zimeandikwa kwa kutumia mtindo wa uhalisiajabu ambao ndicho kiini cha mada ya makala hii. Mtafiti anatambua kuwa, kazi zilizoandikwa kwa kutumia mtindo wa uhalisiajabu ni nyingi. Hata hivyo, kutokana na mawanda, muda, malengo na upeo wa utafiti, isingekuwa rahisi kuzitumia zote. Hivyo, riwaya teule zilitumika kama kiwakilishi cha kazi nyingine za fasihi zinazotumia mtindo wa uhalisiajabu. Data za msingi za makala hii ni sehemu ya data za tasinifu

ya mwandishi ya Shahada ya Uzamivu katika Fasihi yenye mada ya utafiti: "Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili."

## 4.0 Mwega wa Uchambuzi na Nadharia

Uchambuzi, uhakiki na uwasilishaji wa data zilizotumika katika makala hii umetumia mwegamo wa kitaamuli ambao hujikita kuangalia ubora, sifa na tabia za vitu kwa namna watu wanavyotafakari (Kothari, 2004). Mtafiti ametumia mwegamo huu kubaini maana ya dhana husika zilizotumika katika utafiti. Hizi zilimsaidia kwanza, kufafanua sifa na tabia za makundi mbalimbali ya vitu, watu, mandhari na matukio yanayoujenga mtindo wa uhalisiajabu. Pili, mtafiti aliweza kubaini aina mbalimbali za mtindo huo kwa kuzingatia maana inayobeba sifa na tabia za vitu, watu, mandhari na matukio yanayojitokeza ndani ya kazi husika. Mchakato wa kukusanya, kuchanganua na kuwasilisha data ulifanywa kwa njia ya maelezo kwa kutoa ufafanuzi wa makundi husika.

Aidha, nadharia iliyotumika katika uchambuzi na uwasilishwaji wa data katika makala hii ni Uhalisia. Kama inavyoelezwa na Wamitila (2002, 2003) na Njogu na Wafula (2007) nadharia hii ilianza kutumika katika Karne ya kumi na tisa (19). Wamitila (2003) anamtaja George Lukacs (1885 - 1971) kama mmoja wa waasisi wa nadharia hii. Mwanafalsafa huyu alibainisha misingi mikuu mitatu ya nadharia hii ambayo ni kwanza, kazi ya fasihi au sanaa inapaswa kurejelea usawiri wa uhalisi na ukamilifu wake. Pili, ni kuchunguza undani wa picha inavyoonekana katika uhalisi wake. Tatu, ni kugundua sheria za mabadiliko ya kihistoria zinazosababisha mabadiliko fulani katika kazi yoyote ya kisanaa. Msingi wa kwanza wa nadharia hii, ulimwongoza mtafiti katika kutambua wahusika, mandhari na matukio yanayoakisi ukweli wa maisha na yale yanayokiuka uhalisi ambayo yamejengwa katika misingi ya ajabu na hivyo kubaini namna yanavyojenga mtindo wa uhalisiajabu katika riwaya teule. Kutokana na kubaini matukio hayo, mtafiti aliweza kuyapanga katika makundi kutokana na sifa na tabia za wahusika, mandhari na matukio hayo; na hivyo, kubaini aina mbalimbali za mtindo wa uhalisiajabu katika riwaya ya Kiswahili.

## 5.0 Aina za Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya Teule

Vipo vigezo kadhaa vinavyotumiwa na wataalamu wa fasihi kuainisha aina za mitindo mbalimbali ya kazi za fasihi. Miongoni mwa vigezo hivyo ni vile vya kifani, kimuundo, kimtindo, kimaumbo, kidhamira na kimaana (Madumulla, 2009; Wamitila, 2010; Mulokozi, 2017). Hata hivyo, pamoja na kuwapo kwa vigezo hivyo, hakuna kigezo kikamilifu kinachoweza kutumika kuainisha tanzu au mitindo ya kifasihi kwa kadiri inavyojitokeza. Jambo hili linatokana na hoja anazozieleza Wamitila (2010) kuwa kazi ya sanaa hutegemea zaidi msanii anayehusika katika uibuaji wa aina au mitindo mbalimbali ya kifasihi. Aidha, miongoni mwa vigezo tajwa hapo awali, makala hii imezingatia kigezo cha

kimaana katika uainishaji wa mtindo wa uhalisiajabu kwa kuzingatia namna aina hizo zinavyojitokeza katika vitabu husika.

### 5.1 Uhalisiajabu Fantasia

Fantasia ni dhana ya kifasihi inayotumiwa kuelezea kazi za kifasihi zilizo na sifa ya kukiuka uhalisi. Ukiukaji huo hujitokeza kwa namna mwandishi anavyoiumba kazi yake kwa kuikita katika misingi ya kindotondoto ama kutia chuku katika jambo analolisimulia (Khamis, 2007). Lengo kuu la mwandishi huwa ni kutaka kuiaminisha hadhira jambo lisilo la kawaida kwa nia ya kufikisha ujumbe fulani. Kwa kufanya hivyo, msomaji wa kazi inayohusika hushindwa kutofautisha jambo halisi linalosawiri ukweli wa maisha na lile lisilo halisi.

Katika riwaya za Kiswahili za kihalisiajabu, matumizi ya mbinu ya fantasia yamesababisha kuzuka kwa matukio na wahusika wa kihalisiajabu ambao maisha, mienendo na fikra zao zimekitwa katika misingi ya kindoto. Kwa mfano, katika riwaya ya *Nagona*, uhalisiajabu fantasia unajitokeza pale mwandishi anapomjenga mhusika Mimi katika hali ya kindotondoto kiasi cha kumfanya kutokuwa na utambuzi wa baadhi ya mambo yanayotokea katika safari yake. Anasema:

> Yaelekea ilikuwa jioni, maana kulikuwa na mwanga hafifu wa kidhahabu humo bondeni nilimokuwa. Sikumbuki kuona jua na sikumbuki kuona mtu mwingine karibu nami. Labda maruweruwe na usahaulifu ndio ulionifikisha hapa (*Nagona*, uk. 1).

Nukuu hii inabainisha wazi hali ya kutokuwa na utambuzi inayomkuta Mimi katika safari yake. Hajui ni kwa vipi, wala ni saa ngapi amefika mahali alipo. Hii inadhihirika pale anapotumia maneno: "Yaelekea" na "Sikumbuki" katika kubainisha muda. Kimsingi, haya ni maneno yanayotoa picha ya hali ya mhusika huyu kutokuwa na uhakika wala utambuzi wa namna jambo au safari yake ilivyofanyika mpaka kufika mahali alipo. Katika muktadha wa makala hii, hali ya mhusika kutokuwa na utambuzi wa muda, mahali na nini anafanya inadhihirisha namna wanadamu wanavyoyaendesha maisha yao pasipokuwa na mwelekeo au malengo maalumu. Kila analolifanya kwake ni matokeo ya bahati nasibu ambayo hakuwa ameipangilia. Hali hii inasababisha watu kutofikia matarajio yao au kupoteza ndoto zao kwa kukosa mwelekeo au mwongozo sahihi.

Kwa namna nyingine, uhalisiajabu fantasia unatokea katika tukio la utapikaji roho. Hili linafanywa na Mimi na wanafalsafa wakongwe waliofariki miaka mingi iliyopita. Kwa kawaida, ukirejelea hali halisi ya maisha, si rahisi mtu kuitapika roho yake na kisha kuimeza tena na akaendelea kuwa hai. Kutodhihirika kwa tukio hili katika ulimwengu halisi kunasababisha kulitazama tukio hilo kama la kidhahania. Mwandishi anaeleza hili kwa kusema:

> Unawaona hawa, ndiyo waliokuwa askari wa mwanga. Unaviona vitu ving'aavyo kwenye viganja vyao? Hizo ni roho zao. "Roho zao safi!"

> Nilisema kwa mshangao. Bado hazijafikia hata robo ya usafi utakiwao. Usafi wa roho ndiyo sifa muhimu. Haya! Zungumza na roho yako! (*Nagona*, uk. 25).

Mwandishi anatumia mbinu ya kisanaa kusawiri matendo ya ajabu anayoyakuza mno kiasi cha kuvuka uhalisi ili kuiaminisha hadhira kuwa ni mambo ya kawaida. Katika muktadha wa fasihi, mwandishi ametumia tukio hili ili kuwataka wanajamii na hasa viongozi wasio waadilifu kuzisaili dhamira zao kama yale wayatendayo yanaendana na matakwa ya jamii au la! Uchafu wa roho ni kiwakilishi cha matendo maovu kama vile rushwa, unyonyaji, unyanyasaji na ubadhirifu wa mali za umma ambayo mwandishi anawataka viongozi kuepukana nayo ili kufikia malengo na kutekeleza matakwa ya jamii zao.

### 5.2 Uhalisiajabu Tarazi

Katika muktadha wa kifasihi, neno tarazi limefafanuliwa na Wamitila (2003) kuwa ni hali ya upatanifu wa kitabia, lugha, matendo na hali fulani au tabia ya mhusika. Wanaotilia mkazo utarazi, wanaamini kuwa usawiri wa wahusika, mandhari na matukio mbalimbali katika jamii lazima upatanishwe na lugha, matendo na hali, kwa kuzingatia hadhi ya jambo au kitu kinachozungumziwa. Uhalisiajabu tarazi ni mtindo unaohusisha matukio yenye uhalisi na uajabu ndani yake. Matukio hayo huleta upatanifu wa kitabia, maumbile, sifa, hadhi ya mtu au kitu na mahali au mazingira yanayohusika, kwa kuzingatia jambo alilokusudia kulizungumzia mwandishi katika kazi yake.

Katika riwaya ya *Nagona*, uhalisiajabu tarazi umetokana na uhusika wa Mimi kukitwa katika hali ya utatu unaohusishwa na misingi ya imani ya dini za Kikristo. Mfano unajitokeza katika kitabu cha Jimbo Kuu la Dodoma (2017) cha *Katekisimu Yetu* ambacho kinaeleza kuhusu usadikifu wa kuwapo kwa Mungu mmoja aliye katika nafsi tatu. Mwandishi wa riwaya ya *Nagona*, anadhihirisha utatu unaomjenga mhusika Mimi pale anaposema:

> TULIKUWA watatu, EGO, ID na SUPEREGO. Tulikuwa watatu katika mmoja na sauti yetu ilikuwa moja. Kwa wakati huu serikali ilikuwa imetupa kazi ngumu ambayo tulihisi ingetufungulia njia mpya ya kufikiri na kutatua matatizo ulimwenguni (*Nagona*, uk. 31).

Sentensi “Tulikuwa watatu katika mmoja” inadhihirisha wazi suala la umoja na ushirikiano ambao mwandishi anaufungamanisha na imani ya makanisa ya Kikristo kama vile Kanisa Katoliki la Roma na Kanisa la Kilutheri ambayo huamini katika Utatu Mtakatifu, pamoja na dhana zinazotumika katika Nadharia ya Udodosi Nafsi, ambazo ni *Ego*, *Id* na *Superego*. Sifa za kuwapo kwa wingi ndani ya umoja, pamoja na upatanifu wa matendo ya mhusika Mimi yanayosimuliwa katika hali ya wingi, ndizo zinazosababisha kujitokeza kwa mtindo wa uhalisiajabu tarazi katika riwaya ya *Nagona*. Hii ni kwa sababu, sifa hizo zinampa mhusika huyo uhalisi kama inavyotarajiwa kwa mwanadamu wa

kawaida lakini pia zinamwengua katika uhalisi kutokana na hali ya utatu ndani ya umoja anayokuwa nayo. Utatu katika umoja kama unavyotumiwa na mwandishi, unaiwasilisha falsafa pana ya Waafrika kuwa siku zote penye umoja kuna mafanikio. Dhana ya umoja kama mbinu ya mafanikio katika kutekeleza masuala mbalimbali ya kijamii, husawiriwa pia katika semi mbalimbali za Kiswahili. Miongoni mwazo ni "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu," "Kidole kimoja hakivunji chawa" na "Jifya moja haliinjiki chungu."

Uhalisiajabu tarazi mwingine unajitokeza kupitia mhusika Paa. Katika *Nagona*, mwandishi anayahusisha mabadiliko ya Paa na dhana ya ukweli kwamba ni telezi. Mbatiah (1998) anabainisha kuwa sifa kuu ya sitiari ya Paa, Mwanga na *Nagona* ni utelezi wake unaowakilisha ukweli kuhusu maisha. Mwandishi anafananisha sifa za mhusika Paa na zile za Paa mnyama ambaye si rahisi kumkamata kutokana na uwezo wake wa kukimbia. Mabadiliko ya mhusika Paa kutoka katika umbo lake halisi na kuwa katika umbo la msichana yanawakilisha dhana ya ukweli ambao haujibainishi kwa namna moja katika nyakati zote. Mwandishi anaeleza:

> Nilisogea mbele polepole. Nilimfunua Paa kuanzia kichwani hadi miguuni. Alikuwa msichana mzuri ambaye hajapata kuonekana. Nilipomfunua tu muziki ulilia. Aliposimama muziki uliacha... (*Nagona*, uk. 60).

Katika muktadha wa kiujumi, ukweli haufungamani na suala la kiwakati, mazingira wala kipindi fulani. Sifa za mabadiliko anazopewa Paa kutoka katika umbo la mnyama na kuwa msichana mzuri pamoja na utelezi alionao unaomfanya kutoshikika kama ilivyo dhana ya ukweli kutobainika kwa namna moja katika vipindi tofauti, ndizo zinazoujenga uhalisiajabu tarazi katika riwaya ya *Nagona*.

Pia, uhalisiajabu tarazi unajitokeza katika riwaya ya *Bina – Adamu!* Mwandishi anaonesha ukomavu wake katika kuunda dhana anayokusudia kuieleza kwa hadhira kwa kutumia mbinu ya kitarazi. Anaeleza dhana ya utandawazi kwa kuipa sifa ya jitu kubwa ambalo hata Bina Adamu Msafiri anashindwa kuuona mwisho wake. Anasema:

> Niliyatupa macho yangu mbele katika ndoto hiyo maana kweli nilikuwa nimeyafunga, lakini sikuona kitu wala mtu. Niliyaelekeza kushoto, lakini hata huko yalikosa kuambulia chochote. Niliyainua juu. Hatimaye, yalinata juu ya jitu refu lililokuwa na miguu myembamba ajabu; labda likisukumwa tu lingeanguka. Hili lilikuwa pande la jitu nilishindwa kuiona ilikokomea miguu ile miguu ya kiumbe wa ajabu. Lakini, niliweza kuziona pia kucha zake za miguu zilizokuwa kubwa kama masahani (*Bina – Adamu!* uk. 63).

Mwandishi ananasibisha sifa za utandawazi ambao umefanikiwa kuliteka eneo kubwa duniani na kuleta madhara kwa nchi nyingi Barani Afrika, na jitu refu ambalo ukomo wake hauonekani. Urefu wa jitu hilo unahusishwa na ukubwa wa

eneo ambalo utandawazi huo umetapakaa kiasi cha kutobaini mipaka yake. Kucha za jitu hilo zinaashiria mifumo mbalimbali ambayo imefumbatwa katika mgongo wa utandawazi na imekuwa ikileta madhara mbalimbali katika nchi zinazoendelea. Mwandishi anaendelea kutumia uhalisiajabu tarazi pale anapofananisha sifa za utandawazi na namna mfumo huo unavyofanya kazi. Jambo hii linadhihirika pale Jitu anapoeleza:

> Mimi ndiye ninayemiliki maisha yako. Nina uwezo wa kukuchezea ninavyotaka bila hofu ya kudadisiwa na yeyote… Unajua mimi ni kama hydra? Vichwa vyangu ni vingi mno. Nina uwezo wa kufa na kufufuka! (*Bina – Adamu!* kur. 63 - 64).

Katika mfululizo wa mazungumzo haya, mwandishi anaonekana kutilia mkazo namna utandawazi unavyoendelea kuwa tishio, hasa kwa nchi zinazoendelea. Anatumia dhana ya vichwa vingi ili kuonesha namna ambavyo mfumo huo umekuwa ukijibainisha kwa sura mbalimbali kutoka kipindi kimoja hadi kingine. Kichwa kimoja kikikatwa, kingine kinaendelea kuwapo na kuendelea kulipa jitu hilo uhai wa kudumu. Sifa nyumbufu za Jitu, zinafanana na zile za mfumo wa utandawazi ambao umekuwa ukijidhihirisha kwa namna mbalimbali kama vile mfumo wa ukoloni, ukoloni mamboleo na sasa soko huria. Ndiyo maana katika nukuu hiyo, Jitu linaeleza: "Vichwa vyangu ni vingi mno. Nina uwezo wa kufa na kufufuka!"

Hii inamaanisha kuwa dhana ya utandawazi kama ambavyo inajulikana sasa, imekuwapo na itaendelea kuwapo katika sura mbalimbali zenye misingi inayofanana.

### 5.3 Uhalisiajabu Fifi

Kwa mujibu wa TUKI (2004: 80), neno "fifi" maana yake ni "Yenye thamani ndogo; yenye kupoteza hali ya asili; hafifu". Maana inayokaribiana na inayotolewa na TUKI inafafanuliwa na BAKITA (2017: 219) ambao wametafsiri neno "fifi" katika mitazamo miwili. Mtazamo wa kwanza unalifafanua neno hili kuwa ni kitu/mtu au jambo lenye kiwango kidogo cha ubora au thamani. Namna ya pili ni ile inayolitazama neno hilo kuwa ni kitu au jambo lisilokuwa la kawaida; yaani, linalokiuka asili yake. Hivyo, uhalisiajabu fifi ni aina ya mtindo wa uhalisiajabu unaotokana na namna mwandishi anavyowajenga wahusika, mandhari au matukio mbalimbali kwa lengo la kuzua hali fulani ya udhalili unaovuka mipaka ya uhalisi.

Katika kazi za fasihi, uhalisiajabu fifi unaweza kujitokeza kwa namna tatu. Kwanza, ni namna mwandishi anavyowajenga wahusika kwa kuwabadilisha umbo kutoka hali ya utu uzima na kurudi katika hali ya utoto. Kwa namna nyingine, mhusika anaweza kuchorwa akiwa na umbo la utu uzima na kuvishwa fikra za kitoto kiasi cha kuvuka mipaka ya uhalisi wa mambo. Pili, uhalisiajabu fifi unaweza ukajitokeza kutokana na uumbaji wa wahusika fikra, mitazamo na

matendo yanayojengwa katika hali ya kidhalili inayovuka mipaka ya uhalisi wa maisha na kuifanya hadhira kuwatazama wahusika hao kuwa ni wa ajabu. Fikra, mitazamo na matendo ya wahusika hao hukinzana na hadhi ambayo mwandishi anawajengea katika kazi yake. Msingi wa tatu wa uhalisiajabu fifi, unakitwa katika mandhari na matukio mbalimbali yanayosawiriwa katika hali ya kidhalili kiasi cha kuvuka uhalisi wa mambo kama unavyotazamiwa kuwa katika maisha halisi.

Katika riwaya ya *Bina – Adamu!* Uhalisiajabu fifi umejitokeza kupitia tukio la Bina Adamu Msafiri kubadilika viungo vyake vya mwili kutoka hali ya utu uzima na kuwa katika hali ya utoto. Mwandishi anaeleza tukio hilo kwa kuandika:

> Niliangalia mikono yangu ilikuwa ya mtu mzima, lakini vyanda vyake vilikuwa vya mtoto. Nilipigwa na mshangao mkubwa, lakini nikagutuka kuwa nilipokuwa nikiishi na babu nilikuwa mtoto. Labda nilishaanza kukua, lakini kwa nini vyanda vyangu vilibakia kuwa vya mtoto mdogo? Kwa nini? Kwa nini? (*Bina – Adamu!* uk. 22).

Mwandishi anaendelea kubainisha mabadiliko ya Bina Adamu Msafiri kuwa:

> Nilishindwa kuelewa. Sasa niliamua kunyamaza na kuendelea na safari yangu. Kadiri nilivyotembea ndivyo hali yangu ilivyobadilika. Kile kiatu kimoja kilitoweka na hata soksi yenyewe ikapotea. Mikono yangu iliyokuwa ya kitoto iliambukiza sehemu nyingine za mwili kiasi kwamba tulipokuwa tukikaribia ile milima nilikuwa mbilikimo (*Bina – Adamu!* uk. 32).

Mabadiliko ya Bina Adamu Msafiri kutoka umbo la utu uzima hadi kuwa mbilikimo ni mabadiliko yanayomchora mhusika huyo kuwa mhusika wa kihalisiajabu kutokana na uwili wa kimtazamo alionao. Kwanza, ni uhalisi wake kama mwanadamu wa kawaida. Pili, ni uajabu unaotokana na mabadiliko yake, jambo linalokiuka misingi ya uhalisi kama ambavyo Nadharia ya Uhalisia inavyotuelekeza. Katika hali ya kawaida, kadiri mwanadamu anavyokua au siku zinavyopita, ndivyo anavyozidi kujengeka katika viungo vyake kutoka hali ya utoto na kuwa na hali ya utu uzima. Kinyume chake, ni udunishaji wa mhusika ambao unamuweka katika hali ya udhalili na hivyo kujenga mtindo wa uhalisiajabu fifi.

### 5.4 Uhalisiajabu wa Kimajazi

Kietimolojia, neno “majazi” linatokana na kitenzi “jaa” (kujaa) (Ponera, 2014). Maana ya jumla ya kitenzi hicho ni hali ya wingi au ukubwa wa kitu unaofanya kienee katika chombo au mahali fulani. Dhana ya majazi, imefafanuliwa pia na Senkoro (1982) na Madumulla (2009). Wataalamu hao wanakubaliana kuwa, majazi ni aina ya sitiari ambayo inapotaja tu sehemu au sifa ya kitu, hapohapo huashiria au kuwakilisha kitu hicho. Mbinu ya majazi hutumiwa pia kwa upana wa kuelezea muumano uliopo kati ya majina ya mahali, mandhari, sehemu na maana

au wasifu wa sehemu hizo (Wamitila, 2003). Katika makala hii uhalisiajabu wa kimajazi ni aina ya uhalisiajabu unaotokana na uoanishaji wa tabia na sifa, jambo, kitu, mahali, mtu au dhana fulani inayozungumziwa. Majina au vitu hivyo humwelekeza msomaji kwenye wasifu wa tabia, hali ya kitu au mahali na wakati mwingine, namna ya jambo lilivyo.

Katika riwaya za Kiswahili za kihalisiajabu tulizoziteua, uhalisiajabu wa kimajazi umesawiriwa kwa namna mbili. Namna ya kwanza ni ile ambayo mwandishi hutumia majina au dhana zenye maana ya wazi zisizo na mafumbo ndani yake. Namna ya pili ni ile ambayo mwandishi wa kazi inayohusika anatumia majina na dhana zenye maana fiche zinazomuhitaji mtu kuwa na utambuzi na ufahamu wa hali ya juu ili kuweza kubaini maana ya kimuktadha aliyoikusudia.

Katika riwaya ya *Babu Alipofufuka*, uhalisiajabu wa kimajazi unajitokeza pale mwandishi anapotumia dhana ya *mtumaiti* kumrejelea Mzuka. Jina hili ni kielelezo cha mhusika anayezungumziwa na mwandishi. Msomaji wa riwaya hii anapokutana na dhana hii, moja kwa moja anajenga taswira ya mfu ambaye ndani yake, bado kuna uhai. Licha ya kuwa tayari mtu huyu amekwishakufa, bado ana uwezo wa kutenda kama watendavyo watu walio hai. Katika hali halisi, maiti haiwezi kukitwa katika mwendo kama mtu aliye hai. Mwandishi anasema:

> Sikuweza kukuingia kwa sababu ya farakano baina ya maisha yako yanayokimbilia upande mmoja tofauti na wanakokimbilia wengi *maitikwenenda* kama sisi. Dereva wako yuko karibu na mimi kuweza kumuingia kwa urahisi. Ingawa, wewe na mimi ni damu moja umebadilika mno na kuwa mgumu kufikika kwa mwanya mkubwa unaokuza makusudi kila siku (*Babu Alipofufuka*, uk. 21).

Kama inavyodhihirisha katika nukuu hiyo, mwandishi ametumia dhana ya *umaitikwenenda* ili kubainisha falsafa pana ya Waafrika kuhusu dhana ya uhai na kifo. Waafrika wanaamini kuwa mtu hafi moja kwa moja. Mwisho wa maisha yake duniani ni mwanzo wa maisha mengine katika ulimwengu wa wafu hai. Anaihusisha dhana hii na maiti kwa kuipa mwendo kuashiria kuwa ijapokuwa tayari mtu huyo ni maiti, bado yuko katika mwendo, kwani kifo chake duniani si mwisho wa maisha yake, bali ni mwanzo wa maisha mengine katika ulimwengu wa wafu hai.

### 5.5 Uhalisiajabu Tashihisi

Tashihisi ni usemi wenye kukipa sifa ya uhai kitu kisichokuwa na uhai ili kitende au kuonekana kama kina uhai (BAKITA, 2017). Katika makala hii, dhana ya uhalisiajabu tashihisi imerejelewa kama aina ya uhalisiajabu inayotokana na kitendo cha kuhuisha kitu kisicho na uhai kwa kukifanya kiwe na uhai. Katika riwaya ya *Nagona*, uhalisiajabu tashihisi umejitokeza pale mwandishi anapohuisha miti na msitu kwa kuvipa uwezo wa kutenda kama binadamu. Anabainisha hili pale Mimi anapoeleza namna miti na misitu ilivyokuwa ikimcheka na kucheza

kwa kusema:

> Kwa maumivu nilianza kutembelea magoti. Nilisikia vicheko vya watu. Nilijaribu kuongeza mwendo. Nilisikia vicheko kutoka karibu katika kila mti. Msitu mzima ulianza kunicheka. Niliona matawi ya miti yakianza kuchezacheza kwa upepo. Ghafla miti yote iliacha kucheza na vicheko vikaisha. Kukawa shwari (*Nagona*, kur. 1 - 2).

Kama ilivyokwishaoneshwa katika nukuu hiyo, katika maisha halisi, kitendo cha mwandishi kuipa miti na msitu uwezo wa kucheza na kucheka ni kitendo cha ajabu. Kitendo hicho kimesababisha kuzuka kwa uhalisiajabu tashihisi kwa namna mbili. Namna ya kwanza inatokana na uwezo wa miti kucheza, na ya pili ni uwezo wa miti na msitu kucheka. Kama Nadharia ya Uhalisia inavyotuongoza kuwa kazi ya fasihi husawiri yale yanayotokea katika jamii; sifa hizi ni kinyume na uhalisi. Hii ni kwa sababu katika hali ya kawaida, miti haina uwezo wa kucheza wala kucheka bali huweza kutikiswa au matawi yake kuvuma pamoja na mvumo wa upepo, kutikiswa na mtu au kitu.

Kwa upande wa riwaya ya *Bina – Adamu!* uhalisiajabu tashihisi umejitokeza katika kisa cha asili ya kifo cha mwanadamu kinachoelezwa na Bina Adamu Msafiri. Mwandishi anasema:

> Tulisimuliwa na nyanya zamani kabla hajafa. Muumba alimtuma kinyonga aende alikokuwa akiishi binadamu. Alipaswa kumweleza maamuzi yake kuwa ataishi milele na milele. Kinyonga naye mnajua wajukuu zangu ana hatua za polepole. e. e. e… Akatembea kwa mwendo wake wa kawaida. Lakini, baada ya muda, Muumba naye akaghairi. Akaamua kumtuma ndege kwenda kubatilisha ujumbe huo. Yule ndege aliruka kwa wepesi hadi alikokuwa akiishi kwa binadamu. Alimkuta kinyonga akibabatiza maneno yake. "Uliambiwa… a… Ulia… Uli…" Yule ndege akamkatiza. Uliambiwa kuwa utakufa na kuangamia kama mizizi ya msubili!' Huo ndiyo ulikuwa mwanzo wa kifo (*Bina – Adamu!* uk. 27).

Kama inavyobainishwa katika nukuu hiyo, mwandishi anawahuisha kinyonga na ndege kwa kuwapa sifa ya kuzungumza kama binadamu, jambo ambalo ni la ajabu nje ya maisha halisi ya mwanadamu; na hivyo, kuchangia kujenga mtindo wa uhalisiajabu tashihisi. Katika *Babu Alipofufuka*, uhalisiajabu tashihisi unajitokeza pale mwandishi anapoihuisha gari ya K, *Limonsin*, kwa kuipa uwezo wa kutenda kama mwanadamu. Anaeleza:

> *Limonsin* limempembua yule mtu aliyesimama katikati ya njia… Likachukua kasi tena. Kama nalo lilikuwa limepandwa na wazimu. Mbele ya safari sasa harakati zilizidi… Juu nyota zimemezwa na anga la taa lilikwea juu hewani kwa ghadhabu zote lililoweza kukwea nazo. Na ule mwezi ulijazibika na kukimbia juu zaidi, kujificha nyuma ya wingu kwa hasira… Ving'ora vya magari ya polisi vilikuja mfululizo. Ving'ora vya magari ya wagonjwa viliita

kila dakika (*Babu Alipofufuka*, uk. 25).

Matendo ya kibinadamu yanayofanywa na viumbe visivyo binadamu kama inavyoonekana katika nukuu hiyo, ndiyo yanayojenga uhalisiajabu tashihisi. Hii inatokana na ukweli kuwa, si rahisi kiumbe au kitu chochote tofauti na binadamu kufanya matendo sawa na yale anayofanya mwanadamu. Kwa misingi hiyo, vitendo vinavyoelekea kufanywa na viumbe vyenye sifa za kibinadamu kama vile *Limonsin* kupandwa na wazimu, anga kumeza jua na nyota, mwezi kughadhibika na kukimbia vinachangia kujenga mtindo wa uhalisiajabu tashihisi.

### 5.6 Uhalisiajabu Nasibishi

Nasibisha ni dhana inayorejelea uhusishwaji wa vitu viwili au zaidi (TUKI, 2004). Uhusishwaji huu unaweza ukawa wa kitabia, kinasaba na wakati mwingine kimaumbile. Kwa mantiki hiyo, katika makala hii uhalisiajabu nasibishi unarejelewa kama aina ya uhalisiajabu unaojengwa kutokana na ufananishwaji wa kitu kimoja na kingine. Kufanana huko kunaweza kuwa kitabia, kimaumbile, kimatendo, kinasaba, kimatukio au jambo lolote lile linalojenga picha na taswira za ajabu zisizohalisika katika ulimwengu wa kawaida. Katika riwaya ya *Nagona*, uhalisiajabu nasibishi unasawiriwa katika safari ya mhusika Mimi. Mwandishi anatumia barabara ndefu yenye kupindapinda huku ikiwa imezingirwa na milima yenye msitu wa kutisha kuinasibisha na safari ya maisha ya mwanadamu. Katika safari hiyo, anatumia taswira mbalimbali ambazo pia zinachangia kujenga uhalisiajabu nasibishi kwa kuzinasibisha na mambo mbalimbali anayokutana nayo mwanadamu katika maisha yake.

Senkoro (2007) anahusianisha kunasibishwa kwa taswira hizo na misukosuko anayokabiliana nayo mwanadamu wakati wa safari yake ya maisha kwa kueleza kuwa katika taswira na ishara zinazotumiwa na mwandishi; paka mweusi anawakilisha mashaka, wasiwasi na mambo yasiyojulikana katika maisha. Paa anawakilisha uzuri ambao ni wa kupita tu. Jogoo anaashiria kujirudiarudia kwa hali za maisha ambazo ni za kuchusha. Kwa mujibu wa riwaya hiyo, safari hiyo imejengwa kiajabu kwa kuwa ndimo fumbo la maana ya maisha linamopatikana.

Katika *Babu Alipofufuka*, uhalisiajabu nasibishi unasawiriwa katika tukio la mfu hai kujiua na kujifufua tena. Wakati mwingine anajigeuza mchwa na kurejea tena katika umbo la kibinadamu. Tunaelezwa haya katika mazungumzo yafuatayo:

> "Twende…Nataka tu uione dunia nyingine ili ufahamu nini ninachokwambia… Pengine hujui kinachotokea. Umejitenga mno…" Mzuka alikuwa akisema huku akimwongoza K… Baadae, Mzuka akaendelea tena.
> "Tatu nataka ujiue…"
> "Enh!' K moyo uling'ofoka, ukampapa."
> "Ujiue…"

> "Nijiue?"
> "Ndiyo, ujiue! Mwenyewe!"
> Na baadaye K akahisi mikono yake ikinyanyuka pasi na kutaka, na ilipofika shingoni, aliiona inakaba kwa nguvu, bila ya amri yake… Huyo huyo akaanguka chini akafa. Alipokufa lakini, aliweza kusimama tena mwenyewe kwa mwenyewe… Mzuka alimgusa K kichwani, na hapo hapo K aligeuka mchwa. Kisha, yeye, pia, akageuka mchwa... (*Babu Alipofufuka*, kur. 81 - 83).

Mwandishi anainasibisha dhana ya mtu kujiua na kujifufua na dhana ya matabaka kama yanavyojitokeza katika jamii zetu. Kwa kutumia sitiari hiyo, anaielewesha hadhira yake kuwa njia pekee ya viongozi wetu kugundua masaibu yanayowakabili walioko katika tabaka la chini ni kutafuta chanzo cha matatizo hayo; ambacho viongozi hao watakigundua kwa kuzamia kwa undani matatizo na hatimaye kupata ufumbuzi wake. Yote haya yatafanikiwa kwa kuwa na kiongozi anayeweza kushuka daraja la chini kabisa, kukubali kuheshimika kwa kuwaheshimu wengine. Yule anayejua matatizo ya wengine na kukubali kujitolea kuwasaidia. Ndiyo maana Mzuka anamhimiza K kujiua kwanza ili aweze kufika katika ulimwengu wa wafu, ambao kwa muktadha wa kifasihi ni ulimwengu wa watu wa tabaka la chini.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imejadili aina mbalimbali za mtindo wa uhalisiajabu kwa kutoa vielelezo kutoka katika riwaya za *Nagona, Bina – Adamu!* na *Babu Alipofufuka*. Imeonesha kuwa, vipo vigezo kadhaa vinavyoweza kuainisha mtindo wa uhalisiajabu. Aidha, kwa kutumia kigezo cha kimaana, makala imebainisha aina sita za uhalisiajabu. Nazo ni uhalisiajabu fantasia, tarazi, fifi, wa kimajazi, tashihisi na nasibishi. Hata hivyo, aina za mtindo wa uhalisiajabu zinaweza kuwa tofauti na kama zilivyoainishwa katika makala hii kutokana na lengo au kigezo kilichotumika katika uainishaji. Makala inapendekeza kuwa ni muhimu kubaini namna mitindo mbalimbali ya kazi za fasihi inavyoundwa. Hii itasaidia kuuelewa mtindo husika kwa kina na kisha kurahisisha uelewekaji wa maudhui yanayojitokeza ndani yake.

## Marejeleo

Angelus, J. (2019). *Usawiri wa Wahusika wa Kihalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya za Nagona na Mzingile*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

BAKITA (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Faustine, S. (2012). *Matumizi ya Mtindo wa Uhalisiamazingaombwe katika*

*Riwaya Teule za E. Kezilahabi: Dhima na Athari zake kwa Hadhira*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

______ (2017). *Falsafa ya Waafrika na Ujenzi wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

______ (2021) "Umuhimu wa Mtindo wa Uhalisiajabu katika Riwaya ya *Babu Alipofufuka* (2001)". *Kiswahili*. 84 (2): 222-238.

Jimbo Kuu la Dodoma (2017). *Katekisimu Yetu*. Dar es Salaam: F.G.D Tanzania Limited.

Kezilahabi, E. (1990). *Nagona*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Khamis, S.A.M. (2001). *Babu Alipofufuka*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

______ (2007). "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili." *Kioo cha Lugha*. 5: 13-23.

Kothari, C.R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. Toleo 2. New Delhi: New Age International (P) Ltd.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Mbatiah, M. (1998). "Mienendo Mipya katika Uandishi wa Kezilahabi: *Nagona na Mzingile"*. *Mulika*. 24: 1-11.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Ponera, A.S. (2014). *Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Nathari za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

______ (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasinifu.* Dodoma: Central Tanganyika Press.

Senkoro, F.E.M.K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre.

______ (2007). "Uhalisiamazingaombwe katika Fasihi ya Kiswahili: Istilahi Mpya, Mtindo Mkongwe". *Kioo cha Lugha*. 5: 1-12.

TUKI. (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Wafula, M.R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K.W. (2002). *Bina – Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

______ (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Limited.

______ (2010). *Kanzi ya Fasihi*: *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa.